

HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA



TANGAZO

MAOMBI YA KAZI YA UJENZI WA MADARASA NA MABWENI SHULE YASEKONDARI YA KUTWA NACHINGWEA.

Tarehe 01/03/2017 – 14 /03/2017

1. Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya Nachingwea imepokea fedha ya P4R toka Serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa Mabweni mawili na Madarasa matatu Shule ya Sekondari ya Kutwa Nachingwea.
2. Mkurugenzi Mtendaji Hamashauri ya Wilaya Nachingwea anakaribisha maombi kwa wale wote wenye sifa na wanahitaji kufanya kazi hii kama ilivyoainishwa hapo juu, kuleta maombi yao kwa ajili ya kufanyiwa usaili.
3. Sifa za muombaji.
Muombaji anatakiwa awe na sifa zifuatazo:-
 - Awe raia wa Tanzania / aonyeshe Kitambulisho cha mpiga kura
 - Awe na vyeti vya ufundi ujenzi kutoka katika vyuo vinavyotambulika na serikali.
 - Aonyeshe uzoefu wakufanya kazi zinazofanana na kazi hii
 - Aonyeshe mpango kazi wake.(Progam of work)
 - Awe na idadi ya mafundi wasaidizi wasiopungua 5 wenye uzoefu na mafundi wa kada mbalimbali kulingana na kazi husika.

Aidha Majengo yanayotarajiwa kujengwa ni:-

- Mabweni mawili na vyoo.
 - Madarasa matatu
4. Unashauriwa kuiona na kuikagua michoro na kupata taarifa nyingine za kazi hii toka Ofisi ya Mhandisi wa Ujenzi (W).
 5. Tangazo hili linaanza tarehe **01/03/2018** hadi **14/03/2018**.
 6. Mwisho wa kurudisha maombi ni tarehe **14/03/2018** saa **4.00** asubuhi ambapo maombi yote yaliyowasilishwa kwa wakati yatafunguliwa na waombaji waliotimiza vigezo watafanyiwa usaili kuanzia saa **5.00 Asubuhi** katika Ofisi za Mkurugenzi Mtendaji (W)

7. Tafadhalii maombi yote yaandikwe kwa kutumia lugha ya Kiswahili, yafungwe kwa lakiri na yawasilishwe kwa njia ya mkono na sio vingineyo kwa Mkuu wa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea (Ofice Na 20). Jumatatu hadi Ijumaa saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:30 Alasiri.



A.T. KIWALE

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W).

NACHINGWEA

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NACHINGWEA